JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
MKOA WA NJOMBE
HALMASHAURI YA WILAYA YA MAKETE

SHULE YA SEKONDARI KIPAGALO,
S.L.P. 123,
MAKETE.
28-11-2020.

KUMB. NA. KPSS/JI/VOL1/10

NDUGU……

S.L.P……

BULONGWA/MAKETE.

YAH. MAAGIZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA, JANUARI 2019.

Kwa niaba ya Jumuiya ya Shule ya Sekondari Kipagalo, napenda kuchukua nafasi hii kukupongeza kwa kuchaguliwa kwako kujiunga na Shule hii. Kuchaguliwa kwako kumezingatia mafanikio ya ufaulu uliyopata katika kuhitimu Elimu yako ya Msingi.

Ni mategemeo ya Jumuiya ya Shule hii kuwa utaipokea na kuitumia vema nafasi hii adhimu, na kwamba utajituma katika masomo yote na kufaulu vyema katika ngazi hii ya Elimu Ya Sekondari.

Aidha yakupasa kutambua kuwa ushirikiano wako na wenzako, walimu na wafanyakazi wote wa jumuiya hii, juhudi na maarifa na vyote vikiwa vimejikita katika **NIDHAMU** itakuwa ndiyo msingi wa mafanikio yako katika **TAALUMA.**

Masomo yanayofundishwa katika Shule hii ni Elimu ya Uraia(Civics), Kiswahili, Historia(History), Jiografia(Geography), Kiingereza(English Language), Elimu ya Viumbe(Biology), Fizikia(Physics), Kemia(Chemistry) na Hisabati(Basic Mathematics). Masomo yote yanafundishwa kwa lugha ya Kiingereza isipokuwa somo la Kiswahili tu. Utatakiwa kuzungumza lugha ya Kiingereza muda wote uwapo shuleni. Shule hii ni ya kutwa. Wavulana wote watakaa nyumbani kwao na **Wasichana wote watakaa katika Hosteli ya Wasichana iliyopo shuleni**. Nyumba za kupanga kwa wavulana zinapatikana karibu na shule kwa maelewano baina ya wazazi/walezi na wenye nyumba.

Shule itafunguliwa tarehe 11-01-2021 na utapokelewa na **Makamu wa Mkuu wa Shule**. Mara baada ya kufika shuleni utatakiwa kujiandikisha tayari kwa kuanza masomo.

Nakupongeza tena kwa kuchaguliwa kwako. Karibu sana Kipagalo Sekondari.

……

C.E.MUNG'ONG'O.

***MKUU WA SHULE*.**

MAAGIZO MUHIMU KUHUSU MAHITAJI KWA SHULE YA SEKONDARI KIPAGALO

SARE YA SHULE KWA WAVULANA:

1. Mashati mawili (02) meupe mikono mirefu yasiyo na urembo wala kubana, utakaguliwa pindi utakaporipoti.
2. Suruali mbili (02) rangi ya dark blue zenye marinda mawili na turn up, zisiizobana.
3. Sweta rangi ya dark blue shingo ya "V"
4. Viatu vyeusi vya ngozi vya kupigwa kiwi vya kamba (siyo raba au yeboyebo)
5. Socks rangi nyeusi jozi 2
6. Track suit moja ambayo ni nyeusi yenye mistari myeupe mikononi (hii huvaliwa siku za **jumatano** na **ijumaa** ambazo ni siku za michezo).

SARE YA SHULE KWA WASICHANA

1. Sketi mbili(2) zinaoishia magotini mshono wa marinda ya kawaida rangi ya dark blue.
2. Suruali (2) rangi ya dark blue zenye marinda na turn up.
3. Mashati meupe mawili mikono mirefu.
4. Sweta rangi ya dark blue yenye shingo "V".
5. Viatu vyeusi vya ngozi vya kupiga kiwi vya kamba (siyo raba au viatu aina ya yeboyebo).
6. Socks nyeupe jozi 2 (school socks).
7. Track suit moja ambayo ni nyeusi yenye mistari myeupe mikononi (hii huvaliwa siku za **jumatano** na **ijumaa tu** ambazo ni siku za michezo).

VIFAA VYA MICHEZO KWA WANAFUNZI WOTE:

- Raba jozi moja na T-shirt moja kwa wavulana na wasichana rangi ya bluu.
- Bukta moja rangi nyekundu kwa wavulana.

VIFAA VYA TAALUMA:

- Daftari kubwa kumi(10) aina ya **counter book.**
- Kalamu za wino rangi ya bluu au nyeusi za kutosha
- Mkebe mmoja
- Rula,
- Kamusi ya Kiswahili na Dictionary ya Kiingereza.
- Rimu moja ya makaratasi(A4) kwa ajili ya kufanyia mazoezi mbalimbali na mitihani ya kujipima, itakaguliwa shuleni. Fedha haitapokelewa.
- Uje na picha" passport size" zilizopigwa nyuma ya kitambaa cha bluu na shati jeupe nakala 3.
- Faili moja kwa ajili ya kutunza kumbukumbu za kitaaluma.

VIFAA VYA USAFI:

- Kila mvulana aje na jembe moja jipya lenye mpini
- Kila mvulana aje na ndoo moja ya lita 10.
- Kila msichana aje na kwanja moja jipya na mopa moja
- Kila msichana aje na mopa moja.

MAHITAJI YA WASICHANA KWA AJILI YA MATUMIZI YAO WAKIWA KATIKA HOSTEL

1. Godoro moja la futi $2^{1}/_{2}$
2. Mashuka mawili ya rangi ya pinki.
3. Blanketi moja zito.
4. Ndoo 2 za lita 10 kwa ajili ya kufanyia usafi pamoja na kutunzia maji masafi
5. Vifaa vya usafi binafsi k.m. sabuni,mswaki n.k.
6. Taulo moja.
7. Kandambili za kuogea
8. Taa moja ya solar ambayo ataitumia kujisomea usiku(siyo mishumaa)
9. Vyombo vya kulia chakula kama sahani, bakuli, kikombe na kijiko.
10. Sanduku la Bati (tranker) imara kwa ajili ya kutunzia vifaa vyake.
11. Magauni mawili(2) rangi ya zambarau ambalo ni Shamba Dress la kuvaa wakati wa shughuli za nje.
12. Aje na nguo za ndani za kutosha.
13. Aje na 'pedi' (taulo za kike) za kutosha.
14. Aje na bima ya afya kwa ajili ya matibabu awapo shuleni.

HAKIKISHA UMEJAZA FOMU ZIFUATAZO KABLA YA KUJA AU KURIPOTI HAPA:

1. Fomu ya kukubali nafasi
2. Fomu ya maelezo binafsi ya mwanafunzi
3. Fomu ya kupima afya(Medical Examination Form)

JAMHURI YA MUUNGANOWA TANZANIA

OFISI YA ,RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI YA MITAA

MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI

A.

1. jina la mwanafunzi……

2. tarehe ya kuzaliwa……..

3. Mahali alipozaliwa(Wilaya)……(Mkoa)…….

4.Dini…….Dhehebu……

B.

1. jina la mzazi/ MLezi anayekutunza……..

2. Kazi ya mzazi/mlezi……...

3. Anuani ya mzazi/mlezi……

4.Mahali anapoishi mzazi/mlezi…….

Kijiji/Mji…….Kata……..

5.Namba ya simu ya mzazi/ mlezi……

C. Majina ya ndugu wengine wawili wanaohusika na malezi ya mwanafunzi huyo

1. Ndugu……

   Anuani…….

   Namba ya simu……

D.anuani za ofisi ya mtendaji wa Kata au Mwenyekiti wa Mtaa/Kijiji ambako mzazi/mlezi wa mwanafunzi anaishi:

1. Jina la mtendaji wa Kata……..

   Anuani yake…….

   Namba ya simu…….

KIAPO CHA MWANAFUZI

Jina la mwanafunzi…….

Anuani……

Tarehe……

Mimi……nimesoma maagizo ya shule ya sekondari ya Kipagalo kwa makini na kuyaelewa. Naahidi kuwa mwanafuzi mtiifu, na nitazingatia sheria, taratibu za shule kama nitakavyoelekezwa.

KIAPO CHA MZAZI/MLEZI

Mimi……..mzazi/ mlezi wa ……..nimesoma kwa makini maagizo ya shule yaliyotolewa kumhusu motto wangu. Ninakubali kuwa mwanangu achukue nafasi hiyo. Ninaahidi pia kuwa nitashirikiana na uongozi wa shulekatika kumkuza na kumlea mwanafunzi huyu kielimu na kitabia.

Sahihi ya mzazi/mlezi……

Tarehe……

GOVERNMENT OF TANZANIA
REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

THE HEADMASTER,

KIPAGALO SECONDARY SCHOOL,

P.O.BOX 123,

MAKETE.

PART A

To Medical Officer

.....

.....

Mr/Miss.....

(Name in Full)

Please examine the above named person as to his/her physical and mental fitness for a full time schooling course. The examination should include the following categories (1-3) each category or sub-category of which will render the applicant in eligible in case of defect.

1 (a) Eye sight.....
   a. Hearing.....
   b. Limbs.....
   c. Speech.....
   d. Venereal diseases.....
   e. Leprosy.....
   f. Epilepsy.....

2. Neuroses.....

3. Other serious diseases.....

PART B: MEDICAL CERTIFICATE

(To be completed by Government Medical Officer)

I have examined the above named person and consider that he/she is physically fit/unfit ,mentally fit/unfit for a full time schooling course

Date.....Signature.....

Station.....Designation.....

SHERIA ZA SHULE YA SEKONDARI KIPAGALO

1. Mwanafunzi anatakiwa kusimama na kumsalimia mtu yeyote anayemzidi umri wakati wote na mahali popote.
2. Mwanafunzi anatakiwa kuheshimiana na kushirikiana na wenzake.
3. Mwanafuzi anatakiwa na kufanya kazi anazopewa
4. Mwanafunzi anatakiwa kuheshimu bendera ya taifa, wimbo wa taifa, fedha ya taifa wakati wote.
5. Mwanafunzi anatakiwa kuwa msafi na kutunza mazingira vizuri.
6. Mwanafunzi anatakiwa kuwa mfano mwema ndani na nje ya shule
7. Mwanafunzi anatakiwa kuheshimu ofisi ya Mkuu wa Shule,ofisi zote za shule, maktaba pamoja na madarasa
8. Mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria masomo yotekwa wakati na kufanya mitihani inayomhusu .
9. Mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria mikutano yote shuleni kama vile: kupandisha bendera ya taifa, baraza la shule,mikutano ya bweni, darasa n.k.
10. Mwanafunzi anatakiwa kutii kengele kama wito wa haraka.
11. Mwanafunzi anatakiwa kuvaa sare ya shule
    - Darasani
    - Anapotoka nje ya shule
    - Wakati wa Baraza la shule
12. Mwanafunzi atatoka nje ya shule kwa ruhusa maalum ya
    - Mwalimu wa zamuna kuwepo shuleni kabla ya saa 12kamili jioni
    - Mkuu wa shule tu kwa kibali cha kulala nje (kwa wanaokaa hostel)

NB: Mwanafunzi akilala nje ya shule bila ruhusa atakuwa amejifukuzisha shule mwenyewe

13. Mwanafunzi haruhusiwi kutembelea nyumba za walimu na watumishi wengine ila kwa kibali maalum tu. Sehemu hizi ni nje ya mipaka ya shule
14. Mwanafunzi haruhusiwi kuingiza mgeni yeyote katika hostel au darasani
15. Mwanafunzi haruhusiwi kutembelea au kujihusisha na maeneo yafuatayo
    - Vilabu vya pombe
    - Majumba ya kufikia wageni(Guest Houses)
16. Mwanafunzi anatakiwa kutunza mali binafsi pamoja na mali za umma kama vile madawati, vitanda, vifaa vya chakula, vitabu na vifaa vya maabara pamoja na majengo ya shule.
17. Mwanafunzi haruhusiwi kwa namna yoyote kumiliki au kutumia vifaa vinavyotumia umeme awapo shuleni kama vile:
    a) SIMU
    b) JIKO
    c) HEATER
    d) REDIO

MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE

1. Wizi
2. Uasherati, ubakaji na ushoga
3. Uvutaji bangi
4. Kupigana au kumpiga mwalimu au mtumishi
5. Kuoa au kuolewa
6. Kupata au kusababisha mimba ndani na nje ya shule
7. Kutoa mimba
8. Kutoa lugha chafu au ya matusi
9. Kupatikana na makosa ya jinai
10. Kugoma, kuchochea au kuongoza migomo shuleni
11. Kukataa adhabu halali kwa makusudi
12. Kupatikana na simu au vifaa vya simu.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS- TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA MAKETE
SHULE YA SEKONDARI KIPAGALO

MCHANGO WA CHAKULA KWA MWAKA 2021

1. **WASICHANA (KWA MWAKA)**
   - Mahindi debe 6@tshs.15,000/- Jumla 6x15,000/-= TSHS. 90,000/-
   - Maharage debe 2@tshs.40,000/- Jumla 2x40,000/- = TSHS. 80,000/-
   - Mchele debe 1@tshs.40,000/- jumla 1x40,000/- = TSHS. 40,000/-

   JUMLA NDOGO TSHS. 210,000/-

2. **WAVULANA KWA MWAKA**
   - Mahindi debe 3@tshs.15,000/- Jumla 3x15,000/- = TSHS. 45,000/-
   - Maharage lita 10@tshs.2000/- Jumla 10x2000/- = TSHS. 20,000/-
   - Mchele 1debe @tshs 40,000/- Jumla1 x40,000/- = TSHS. 40,000/-

   JUMLA NDOGO TSHS. 105,000/-

3. **GHARAMA NYINGINE**
   - Kulipa Wapishi……THSH. 10,000/-
   - Kununua sukari…… TSHS. 7,000/-
   - Kukoboa na kusaga……TSHS. 6,000/-
   - Mafuta ya kupikia…… TSHS. 7,000/-
   - Mboga za majani na viungo…… TSHS. 5,000/-
   - Nyama…… TSHS. 7,000/-
   - Vyombo vya kupikia …… TSHS. 3,000/-
   - Kuni za kupikia…… TSHS. 10,000/-

   JUMLA YA GHARAMA NYINGINE TSHS. 55,000/-

   N.B. Wasichana watachangia tshs. 15,000/- kwa mwaka kwa ajili ya kumlipa Matron.

JUMLA KUU/JUMLA YOTE

(a) Wasichana…… **TSHS. 280,000/-**
(b) Wavulana……**TSHS. 160,000/-**

N.B. Bei elekezi ya nafaka zilizotajwa hapo juu inaweza kubadilika kuendana na mwenendo wa hali ya soko.

Nakutakia utekelezaji mwema kwa maendeleo ya watoto wetu.

……

CHRISTOPHER E. MUNG'ONG'O
MKUU WA SHULE-(0765866357)
Kwa niaba ya kamati ya Chakula